

NEW



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MJI GEITA



12/08/2022

## TANGAZO ! TANGAZO ! TANGANZO !

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI GEITA  
ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE WENYE SIFA KUOMBA  
NAFASI ZIFUATAZO;

### 1. WACHUNAJI WA MIFUGO NA WAOSHA UTUMBO

SIFA :-

- I. AWE RAIA WA TANZANIA.
- II. AWE ANAJUA KUSOMA NA KUANDIKA.
- III. AWE NA UJUZI WA KUFANYA KAZI KWENYE MACHINJIO. KUCHUNA NGOZI ZA NGÓMBE, MBUZI NA KONDOO, KUONDOA UTUMBO, KUFANYA USAFI WA NDANI YA MACHINJIO NA MAENEO YANAYOZUNGUKA MACHINJIO.
- IV. AWE NA AKILI TIMAMU
- V. KWA WACHUNAJI AWE NA LESENI
- VI. AWE NA CHETI CHA UTHIBITISHO WA AFYA KUTOKA TAASISI ZINAZOTAMBULIKA NA SERIKALI
- VII. AWE NA UMRI USIOPUNGUA KUANZIA MIAKA 18 – 40
- VIII. ASIWE NA HISTORIA YA KUSHIRIKI KUTENDA MAKOSA YA JINAI.

## 2. MAJUKUMU YA KAZI ALIYOOMBA

- i. Kutoa mifugo inoyokusudiwa (Ng'ombe, Mbuzi na Kondoo) kuchinjwa kutoka kwenye eneo walipohifadhiwa (Lairage) na kupelekwa kwenye Machinjio.
- ii. Kuchuna ngozi kwa Ng'ombe, Mbuzi na Kondoo baada ya kuchinjwa na kukaushwa damu
- iii. Kuhakikisha ngozi zilizochunwa zinapelekwa eneo mahususi lililokusudiwa
- iv. Kuhakikisha matumbo yanatolewa na kupelekwa eneo lililokusudiwa kwa ajili ya kusafishwa.
- v. Kusafisha utumbokwa maji safi na salama na kisha kupeleka eneo lililokusudiwa kwa ajili ya kukabidhiwa mteja
- vi. Kusafisha vyombo na vifaa vilivyotumika katika kusafirisha matumbo, kuchuna ngozi pamoja na eneo lililokuwa kutumika kuosha matumbo
- vii. Kupima nyama kwenye mzani na kuandika kilo za nyama kwenye leja
- viii. Kuhakikisha nyama iliyochiniwa na viungo vvote vva ndani anakabidhiwa mteja baada ya kuidhinishwa na mkaguzi wa nyama (meat inspector)

### 1. KAZI YA KUFANYA USAFI (NAFASI 3.)

#### • SIFA

- i. Awe Mtanzania
- ii. Awe anajua kusoma na kuandika
- iii. Awe na uwezo wa kufanya usafi ndani na nje ya mchinjio.
- iv. Awe na cheti kilichothibitishwa afya yake kutoka taasisi zinazotambulika na Serikali.
- v. Awe na akili timamu.
- vi. Asiwe na historia ya kushiriki makosa ya jinai.
- vii. Awe na umri usiozidi miaka 40.

## 2. MAJUKUMU


- i. Kufanya usafi ndani na nje ya jengo la machinjio
- ii. Kusafisha na kutunza vifaa vinavyotumika kwenye usafi
- iii. Kukusanya uchafu na kupeleka eneo lililokusudiwa
- iv. Kuzoa mbolea na kupeleka sehemu husika
- v. Kupeleka vifaa vya usafi mara baada ya kutekeleza majukumu eneo utakaloelekezwa (store).

New

- Maombi yatumwe kwenye anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi,  
Halmashauri ya Mji,  
S.L.P 384,  
**GEITA.**

- Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **19/08/2022**  
(9.30 Mchana).



Zahara Michuzi  
**MKURUGENZI**  
**HALMASHAURI YA MJI**  
**GEITA**

MKURUGENZI  
HALMASHAURI  
GEITA.



Jiandae kuhesabiwa siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022